پُراسرار بھکاری

OMBA OMBA WA AJABU

(SWAHILI)

Shaykh-e-Tariqat, Ameer-e-Ahl-e-Sunnat
Founder of Dawat-e-Islami, Allamah Maulana Abu Bilal
MUHAMMAD ILYAS
Attar Qadiri Razavi

پُراَسرار بِھکارِی

Purasrar Bhikari

OMBAOMBA WA AJABU

Kitabu hiki kimeandikwa na Sheikh-e-Tarīqat Amīr-e-Aĥl-e-Sunnat, muasisi wa Dawat-e-Islami ‘Allāmaĥ Maulānā Abu Bilal Muhammad Ilyas Attar Qadiri Razavi دَامَتْ بَرَكَاتُهُمُ الْعَالِيَه kwa kiUrdu. Kikatafsiriwa na Majlis Tarajim kwa Kiswahili. Ikiwa utakipata na makosa yoyote, tafadhali wajulishe Majlis kwa kutumia anwani ya posta au barua pepe ifuatayo kwa nia ya kupata thawabu.

Majlis-e-Tarājim (Dawat-e-Islami)

Aalami Madani Markaz, Faizan-e-Madinah, Mahallah Saudagran, Purani Sabzi Mandi, Bab-ul-Madinah, Karachi, Pakistan

UAN: ☎ +92-21-111-25-26-92 – Ext. 1262

Barua pepe: ✉ translation@dawateislami.net

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ وَ الصَّلٰوةُ وَ السَّلَامُ عَلٰى سَيِّدِ الْمُرْسَلِيْنَ
اَمَّا بَعْدُ فَاَعُوْذُ بِاللّٰهِ مِنَ الشَّيْطٰنِ الرَّجِيْمِ ؕ بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ؕ

Du’a Kabla ya Kusoma Kitabu

Soma dua ifuatayo kabla ya kusoma kitabu au somo la kidini. اِنْ شَآءَاللّٰه عَزَّوَجَلَّ utakumbuka yote uliyoyasoma:

اَللّٰهُمَّ افْتَحْ عَلَيْنَا حِكْمَتَكَ وَانْشُرْ
عَلَيْنَا رَحْمَتَكَ يَا ذَا الْجَلَالِ وَالْاِكْرَام

Tafsiri

Ee Mola عَزَّوَجَلَّ ifungue milango ya elimu na busara kwa ajili yetu, na utuhurumie! Ewe uliye Mtakatifu kabisa.

(Al-Mustatraf, juz. I, uk. 40, Dar-ul-Fikr, Beirut)

Kumbuka: Msalie Mtume صَلَّى اللّٰهُ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم mara moja kabla na baada ya dua.

Transliteration Chart

ء	A/a	ڑ	Ř/ř	ل	L/l
ا	A/a	ز	Z/z	م	M/m
ب	B/b	ژ	X/x	ن	N/n
پ	P/p	س	S/s	و	V/v, W/w
ت	T/t	ش	Sh/sh		
ٹ	Ṫ/ṫ	ص	Ṣ/ṣ	ھ/ ہ /ۃ	Ĥ/ĥ
ث	Š/š	ض	Ḍ/ḍ	ی	Y/y
ج	J/j	ط	Ṭ/ṭ	ے	Y/y
چ	Ch	ظ	Ẓ/ẓ	◌َ	A/a
ح	Ḥ/ḥ	ع	‘	◌ُ	U/u
خ	Kh/kh	غ	Gh/gh	◌ِ	I/i
د	D/d	ف	F/f	و مدّہ	Ū/ū
ڈ	Ḋ/ḋ	ق	Q/q	ی مدّہ	Ī/ī
ذ	Ż/ż	ك	K/k	ا مدّہ	Ā/ā
ر	R/r	گ	G/g		

YALIOMO

Du'a Kabla ya Kusoma Kitabu ii
Transliteration Chart..... iii

Ombaomba wa ajabu 1

Ubora wa kumsalia Mtume ﷺ.....1
1. Utajiri unaweza kununua dawa lakini hauwezi kununua tiba! 6
2. Miale ya moto na moshi kutoka kaburini 8
Haikubaliwi sadaka itokanayo na mapato ya haramu.....9
Maangamizi kutokana na tonge ya chakula cha haramu....10
3. Kaburi lililobetabeta 10
Atarushwa Motoni 11
4. Maiti alikaa kitako 11
Uovu wa riba.....12
5. Kaburi lilikuwa limejaa nge.....13
Tumo kutokana na kunyoa ndevu ni haramu.....14
Hukumu ya uislamu kuhusu mali ya haramu 14
Baraka za Madanī kwa kujitolea kikweli kweli 15

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ وَالصَّلٰوةُ وَالسَّلَامُ عَلٰى سَيِّدِ الْمُرْسَلِيْنَ
اَمَّا بَعْدُ فَاَعُوْذُ بِاللّٰهِ مِنَ الشَّيْطٰنِ الرَّجِيْمِ ؕ بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ؕ

Ombaomba wa ajabu*

Hata shetani akakutia uvivu wa aina gani kusoma kitabu hiki, kisome chote ili upate habari za kushangaza.

Ubora wa kumsalia Mtume ﷺ

Mtume wa Raḥmaĥ, Mtetezi wa Ummaĥ, Mmiliki wa Pepo صَلَّى اللّٰهُ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema, “Enyi watu! Hakika atakayesamehewa haraka kutokana na adhabu na mateso ya Siku ya Kiyama ni yule aliyenisalia kwa wingi duniani.” *(Firdous-ul-Akhbār, Juz. 5, uk. 375, hadithi 8210)*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب　　صَلَّى اللّٰهُ تَعَالٰى عَلٰى مُحَمَّد

Mtu mmoja alieleza: Nilikwenda Madīnaĥ-tul-Auliyā (Mji wa Mawalii), Multan Sharīf na nikazuru ziyara ya Ghauš Baĥā-ul-Ḥaq Waddīn Zakarīyā Multānī قُدِّسَ سِرُّهُ النُّوْرَانِي. Nilipokuwa nikitoka

* Kisa hiki kiliripotiwa na gazeti la Gujrātī siku chache zilizopita. Nilikiona kinashtua watu; kwa hivyo ninaeleza ninayoweza kuyakumbuka. Kuna marekebisho machache na maelezo ya ziada ili ndugu waislamu wapate mafunzo kutokana nacho.

[Sag-e-Madīnaĥ عُفِيَ عَنْهُ]

baada ya kutia Fatiḥa, nilishtuka nilipomuona mtu mmoja mwembamba na mrefu aliyekuwa akishughulika kutoa dua amefunga ndoo shingoni mwake na vidole vya mkono wake wa kulia amevitumbukiza ndani. Uso wake ulionesha kuwa alikuwa na mateso mazito. Nilipomtazama kwa karibu, uso wake haukuwa mgeni kwangu. Nilimgojea mpaka akamaliza dua, halafu nikamfuata na kutoa salamu. Akaitikia, akanitazama kwa makini. Alinitambua na akatabasamu kidogo, mara tabasamu hiyo ikatoweka. Akazama katika majonzi tena. Nikamuuliza sababu ya yeye kufunga ndoo shingoni na kutumbukiza vidole vyake ndani. Alivuta pumzi na akasema:-

“Nina duka dogo la reja reja. Wakati mmoja omba omba alikuja kuniomba pesa. Nikampa shilingi. Aliipokea kwa shukrani na kabla ya kuondoka akaniombea dua. Siku ya pili, akaja tena. Basi, akafanya mazoea ya kuja. Ikawa kila akija huwa nampa chochote. Wakati mwengine alikaa na kunieleza masaibu yake ya maisha ambayo yalinifanya nimuhurumie. Urafiki wetu ukakita mizizi na usuhuba ukaendelea kwa muda. Mara akakosa kuja kwa siku kadhaa, jambo ambalo halikuwa desturi kwake. Nilishikwa na wasiwasi, nikawaza, huenda akawa ni mgonjwa. Nilikumbuka kuwa alikuwa akiishi peke yake katika kijumba kando na mji. Nilifanya bidii kumtafuta. Mwishowe nilimpata katika kijumba chake. Nilipoingia ili nimuone, nilikuta matambara yametapakaa sakafuni na vyungu vilivyovunjika pembeni. Kwa ufupi nyumba ilionesha umaskini na ulitima wa ajabu! Alikuwa amelalia kitanda kibovu kilichokuwa pembeni mwa chumba.

Alikuwa mgonjwa sana. Hali yake ilionesha kuwa hawezi kupona. Nilitoa salamu. Nikasimama karibu yake. Aliponiona, alichangamka na akaniomba nikae karibu naye. Alizungumza kwa sauti ndogo tena kwa tabu, “Ndugu! Nisamehe kwa ujanja niliokufanyia.” Nikamuuliza, “Nini?” Akasema, “Visa vyote vya huzuni nilivyokuelezea, havikuwa vya kweli. Nilikuwa nikitoa visa hivyo kwa watu ili nipate pesa. Kwa sababu sina uhai tena nataka nikufunuliye yote.

Ninatoka katika familia inayojiweza na niliishi maisha mazuri. Nilikuwa nimeoa na nilikuwa na watoto kadhaa. Baadaye uvivu ukaniingia nikashindwa kufanya kazi. Nikawa najikalia bure. Hatimaye uraibu wa kuomba omba ukaniingia na nikakufanya kuomba ndiyo kazi yangu. Mke wangu aliichukia kazi hii na mara kwa mara tuligombana. Wakati ulipita na wanangu wakawa watu na kazi zao za kuheshimika. Wao pia hawakupendezwa na maisha yangu ya izara. Walinilazimisha kuiacha kazi hiyo lakini nilikuwa nimeshaizoea. Hatimaye, hamu ya kupata pesa za bwerere ilinivaa na kunifanya niitoroke familia yangu na kuishi peke yangu katika mahali hapa palipo na upweke.” Halafu akaashiria kipembeni palipokuwa na mrundo wa matambara. Akasema, “Ondoa matambara, utapata chini yake magunia manne. Fungua lolote.” Nilipofungua tu, nilipigwa na butwaa! Gunia lilikuwa limefurika mabunda ya noti! Omba omba huyu kwangu mimi alikuwa mtu wa ajabu! Akasema, “Magunia haya yote manne yamejaa noti. Ndugu! Nimekuamini na kukupa siri kubwa ya maisha yangu na sasa jukumu lako ni kutimiza

wosia wangu." Nikakubali. Akasema, "Angalia! Daima nimekuwa na mapenzi makubwa ya mali haya. Kwa sababu yake nimepoteza familia yangu. Si kula wala kuvaa vizuri. Raha yangu ilikuwa ni kutazama pesa hizi!"

Akatulia kidogo na akasema; "Niletee mabunda machache ya noti ili niyakumbatie na kuyabusu." Nilichukua mabunda kadhaa kutoka guniani na kumpa. Ghafla macho yake yalikoboka. Akashika bunda moja baada ya jingine na kulibusu huku mikono inamtetemeka. Halafu akayakumbatia mabunda ya noti kwa shaki. Akasema, "Huu ni wosia wangu, itabidi uutimize kwa vyo vyote. Nataka utajiri wangu wote uzikwe pamoja nami." Nikatoa ahadi kufuata wosia wake. Alipokuwa akizibusu noti kwa hamu kubwa, ghafla sauti kali ya kutisha ikamtoka kooni mwake. Mikono yake iliziachilia noti, zikaanguka sakafuni. Kichwa chake kikalemea upande mmoja. Roho ikamtoka. Nilitetema kwa uoga.

Nilijikaza na kwa haraka nikaziokota zile noti zilizokuwa zimeenea kifuani pake na sakafuni, nikaziregesha guniani. Nikalifunga gunia na nikalificha kwenye rundo la matambara. Nilisaidiwa na watu kumzika katika kaburi kubwa. Nilifaulu kutumbukiza magunia ndani ya kaburi bila ya wao kujua.

Baada ya kipindi kifupi, nikaanza kupata hasara katika biashara yangu na kuwa na madeni makubwa. Wanaonidai walitaka pesa zao mara kwa mara lakini si kuweza kuwalipa. Siku moja nikamkumbuka rafiki yangu 'Omba omba wa ajabu'. Nilijiona mjinga. "Kwa nini nilimzika pamoja na mali yake? Ni wazi

pesa hizo hazitamfaa kaburini. Lau ningebakia nazo, ningekuwa tajiri mkubwa hivi sasa." Shetani akaanza kunighilibu kwenda kuzichukua. "Siri hii niliificha sikumwambia mtu yeyote. Pesa lazima ziwe bado zimo mle mle kaburini." Mawazo haya yalinivutia mno na nikashawishika kwenda kuziiba kutoka kaburini.

Usiku mmoja nilikwenda maziyarani na vifaa vya kufukua kaburi. Nilipokuwa nimesimama kando ya kaburi lake, kimya cha kutisha kilikuwa kimetanda na moyo ulinidunda dunda kwa hofu. Mwili nao ulikuwa umelowa jasho. Hatimaye, nilijishajiisha na nikaanza kufukua kaburi. Pole pole nikapata nguvu na nikazidi kuchimba mpaka nikalifukua kaburi. Nilichohitaji ni kutia mkono kaburini lakini nikaingiwa na uoga tena. Nikaanza kutetema tena kwa ajili ya hofu. Mawazo ya kutisha yakanijia. Moyo wangu ulinishawishi kwa nguvu kuregea na kunizuia kuharibu maisha yangu ya baadaye kwa kuchukua pesa za haramu. Lakini tamaa ikanishinda na hamu ya kupata pesa ikanishawishi kuendelea. Tamaa kubwa ya pesa ilinisahaulisha madhara na nikatia mkono wangu wa kulia kaburini. Nilipokuwa napapasa kutafuta gunia la pesa, mkono wangu uligusa kaa la moto. Nilipiga ukemi kwa ajili ya maumivu makali. Kwa haraka niliutoa mkono wangu kaburini na nikachomoka mbio.

Mkono wangu ulichomeka vibaya. Nililia na nikamuomba Allah عَزَّوَجَلَّ msamaha lakini maumivu hayakuweza kuondoka. Nimetembelea madaktari na mahakimu wengi lakini bado sijaweza kupata afueni. Isipokuwa nikitia vidole vyangu katika

maji ndiyo hupata nafuu. Ndiyo maana naweka mkono wangu majini wakati wote. Kisa hicho cha kuhuzunisha kilinifanya ni uchukie ulimwengu zaidi. Na nikakumbuka aya ifuatayo ya Qur'ān Tukufu:

بِسۡمِ اللّٰهِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِيۡمِ

اَلۡهٰكُمُ التَّكَاثُرُ ۙ﴿۱﴾ حَتّٰى زُرۡتُمُ الۡمَقَابِرَ ؕ﴿۲﴾

Kwa jina la Allah (عَزَّوَجَلَّ), Mwingi wa Rehema, Mwenye kurehemu kumekushughulisheni kutafuta wingi mpaka muje makaburini.

(Tafsiri ya Qur'an, Sūrah At-Takāsir, aya 1 & 2)

Ndugu waislamu! Hebu tafakarini kuhusu maangamizi yanayoletwa na tamaa kubwa ya mali. Omba omba alikufa huku anabusu pesa zake za haramu na rafiki yake aliyekwenda kuchukua pesa zile akaingia matatani. Allah عَزَّوَجَلَّ awasamehe na awaondolee madhambi yao bila hisabu. Na sisi pia atusamehe madhambi yetu.

اٰمِيْن بِجَاهِ النَّبِيِّ الْاَمِيْن صَلَّى اللهُ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم

1. Utajiri unaweza kununua dawa lakini hauwezi kununua tiba!

Ndugu waislamu! Tunaweza kujifunza maua mengi ya Madanī ya hekima kutokana na kisa hiki. Wale ambao wanatamaa nyingi

ya kukusanya pesa, wale ambao hawapambanui kati ya haramu na halali, wale ambao wanaacha sala ya jamaa kwa ajili ya biashara, bali mara nyingine hata huacha sala yenyewe (مَعَاذَ اللّٰه عَزَّوَجَلَّ) na wale wanaotafuta utulivu katika pesa tu, katika kisa hiki kuna mazingatio makubwa kwa ajili yao. Kumbuka, utajiri unaweza kununua dawa lakini hauwezi kukutibu! Pesa zinaweza kukuletea marafiki lakini haziwezi kukuletea uaminifu! Utajiri unaweza kukusabishia kifo lakini hauwezi kukusaidia kuzuia mauti. Utajiri unaweza kukuletea umaaarufu lakini hauwezi kukuletea heshima.

Ndugu waislamu! Wale ambao wamefanya kuomba omba ni kazi yao wanafaa kuzingatia kisa hiki cha kutisha cha 'Omba omba wa ajabu'. Kumbuka tabia ya kuomba ni haramu itakayokutia motoni! Anayeomba bila ya sababu ya sharia, ajitafutia moto. Na kila akipata pesa zaidi kwa njia hiyo, anajiongezea adhabu ya moto. Soma hadithi hizi nne kuhusu tabia ya kuomba omba:

1. Anayeomba watu wakati hafi na njaa wala hana familia kubwa ambayo imemshinda kusimamia atafufuliwa bila nyama usoni mwake Siku ya Kiama. *(Shu'ab-ul-Imān, juz 3, uk. 274, hadithi 3526)*

2. Anayeomba bila ya dharura, ni mfano wa yule anayekula kaa la moto. *(Al-Mu'jam-ul-Kabīr, juz. 4, uk. 15, hadithi 3506, Dār Iḥyā-ut-Turāš-ul-'Arabī, Beirut)*

3. Anayeomba ili aongeze utajiri wake, anajiombea makaa ya moto kwa hivyo muache aombe kidogo au kingi. *(Ṣaḥīḥ Muslim, uk. 518, hadīthi 1041, Darār Ibn-ul- Ḥazm, Beirut)*

4. Mwenye kuomba watu ili kujitajirisha, basi ile (mali) ni jiwe la moto la Jahanam. Akitaka aombe kidogo au kingi. *(Al-Iḥsān bittartīb, Ṣaḥīḥ ibn-e-Ḥabbān, Juz. 5, uk.166, hadithi 3382, Dār-ul-Kutub-ul-'Ilmiyyaĥ, Beirut)*

2. Miale ya moto na moshi kutoka kaburini*

Alikuwa kila siku akisali sala zote tano za faradhi kwa wakati wake. Mbali na kuwa tajiri, alikuwa karimu. Aliwasaidia maskini na wajane. Hata aliwalipia mayatima mahari. Pia alikuwa ametekeleza ibada ya Hajj. Asubuhi moja ya mwaka wa 1973, akafariki. Watu wengi walihudhuria mazishi yake kwa sababu alipendwa na kujulikana na watu wengi. Kaburi lilikuwa tayari na mwili wake ulikuwa karibu kutiwa ndani. Mara kukatokea jambo la ajabu! Kaburi lilifungika!!! Kila mmoja alishangaa. Kaburi likachimbwa tena. Walipokuwa tayari kumtia ndani, likajifunga tena! Watu wakajaribu kuchimba jingine lakini matokeo yakawa ni yale yale. Hatimaye walifaulu kumzika walipojaribu kwa mara ya nne. Baada ya kutia fatiha, watu wakageuka kuregea zao nyumbani. Hatua chache kutoka kaburini, ardhi ikaanza kutikisika. Walishtuka, wakageuka

* Kisa hiki cha kutisha ni cha kweli na kilichapishwa katika jarida la Nawā-e-Waqt. Nina kihadithia kwa maneno yangu ili ndugu waislamu wapate funzo kutokana nacho. [Sag-e-Madīnaĥ عفی عنہ]

kuangalia, wakaona mandhari ya kutisha. Nyufa zilikuwa zimetoka kaburini; miale ya moto ilitoka ndani. Vilio na mayowe yalisikika kutoka kaburini. Watu wote waliingiwa na hofu wakakimbia haraka iwezekanavyo. Watu walishangaa, vipi mtu mcha Mungu, karimu na mwenye kuheshimika kama yule anaweza kuadhibiwa. Walipouliza kuhusu maisha yake ya zamani, waligundua kuwa marehemu alikuwa mwerevu mno tangu utotoni mwake na akapata elimu ya juu. Alipomaliza masomo, alihongana ili apate kazi katika ofisi ya serikali. Akawa mraibu wa hongo. Alinunua mali nyingi akitumia pesa hizo za haramu. Akaenda Ḥajj kwa pesa hizo na ukarimu wake wote unatokana na pesa hizo za haramu. Tunajilinda kwa Allah عَزَّوَجَلَّ kutokana na ghadhabu yake.

Ndugu waislamu! Mumeona matokeo ya kukusanya mali ya haramu? Kumbuka! Kulingana na hadithi, anayehonga na anyehongwa wote wataingia motoni. *(Al-Mu'jam-ul-Awsaṭ lil-Ṭabarānī, Juz. 1, uk. 550, hadithi 2026, Dār-ul-Kutub-ul-'Ilmiyyaĥ, Beirut)*

Haikubaliwi sadaka itokanayo na mapato ya haramu

Matendo mema yatokanayo na haramu hayana faida kwa sababu Allah عَزَّوَجَلَّ ametakasika na anakubali tu vile vilivyotakasika. Kipenzi cha Allah عَزَّوَجَلَّ, Rehema ya ulimwengu صَلَّى اللهُ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema, "Anayechuma mali ya haramu na aitoe sadaka, haitokubaliwa. Atakachotumia hakitakuwa na baraka na atakachokiacha ulimwenguni kitakuwa ni njia ya kuingia Motoni." *(Sharḥ-us-Sunnaĥ-lil-Baghwī, juz 4, uk. 205-206, hadithi 2023, Dār-ul-Kutub-ul-'Ilmiyyaĥ, Beirut)*

Maangamizi kutokana na tonge ya chakula cha haramu

Imehadithiwa kwamba tonge moja ya chakula cha haramu ikiwa tumboni mwa mwanadamu, kila malaika ardhini na angani atamlaani yeye kwa kipindi ambacho chakula hicho kitabakia tumboni na akifa kikiwa tumboni, makazi yake yatakuwa Motoni. *(Mukāshafa-tul-Qulūb, uk. 10, Dār-ul-Kutub-ul-'Ilmiyyaĥ, Beirut)*

3. Kaburi lililobetabeta

Tarehe 27 mfungo saba (Jumadil Awwal) 144 Hijri, mwili wa askari uliletwa kuzikwa katika maziyara ya Ratta-Amral mjini Rawalpindi. Alipokuwa akizikwa, kaburi likabetabeta! Mara ya kwanza, watu wote walimlaumu mchimba kaburi kwa hivyo wakachimba jengine. Mwili wake ulipokuwa unatiwa kaburini, kaburi likabetabeta tena! Watu wakaingiwa na wasiwasi na hofu. Jambo hili likafanyika tena kwa mara ya tatu, kaburi lilibetabeta mno hata kumzika ikawa haiwezekani. Watu wote wakamuombea dua ya msamaha na wakaamua kwamba lazima wamzike kwa njia yoyote. Kwa hivyo, ingawa kaburi walilolichimba tena lilikuwa limebetabeta, waliulazimisha mwili kaburini na wakafaulu kumzika. Tunajilinda kwa Allah عَزَّوَجَلَّ kutokana na ghadhabu yake.

Ndugu waislamu! Kunamazingatio makubwa kutokana na kisa cha kutisha cha askari. Allah عَزَّوَجَلَّ ndiye anayejua zaidi dhambi ambayo imemfanya awe ni funzo kwetu. Wanaotafuta vyeo na umaarufu wasome kwa makini riwaya ifuatayo:

Atarushwa Motoni

Sayyidinā ʻAbdullāĥ Ibn-e-ʻAbbās رَضِیَ اللّٰہُ تَعَالٰی عَنْہُمَا amesimulia kwamba Mtume Mtukufu صَلَّی اللّٰہُ تَعَالٰی عَلَیْہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم amesema, “Mtu ambaye alikuwa mtawala juu ya zaidi ya watu kumi na akatoa hukumu katika kesi zao; (bila ya kuzingatia) iwapo watu waliridhia au hawakuridhia hukumu yake, ataletwa Siku ya Kiama mikono yake ikiwa imefungwa shingoni mwake. Ataokolewa tu, ikiwa alitoa hukumu kwa mujibu wa hukumu za Allah عَزَّوَجَلَّ na hakuchukua hongo wala hakupendelea katika hukumu zake. Ikiwa atakuwa amekwenda kinyume na hukumu ya Allah عَزَّوَجَلَّ, amechukua hongo na kutoa hukumu yenye kupendelea upande mmoja, mikono yake itafungwa pamoja na atarushwa Motoni. Moto ambao hataweza kufika chini yake hata baada ya miaka 500.” *(Al-Mustadrak lil-Ḥakīm, juz. 05, uk. 140, hadithi 7151, Dār-ul-Ma’rifaĥ, Beirut)*

4. Maiti alikaa kitako

Soma kisa hiki cha kutisha cha mfanyabiashara wa nguo Jawĥar-Ābād (Tando Adam, Pakistan) na uogope ghadhabu ya Allah عَزَّوَجَلَّ: Kwa mujibu wa taarifa za gazeti, maiti aliletwa maziyarani. Imamu alipoanza kumsalia, maiti alikaa kitako! Watu waliogopa na kukimbia. Imamu pia akaacha kusali na akasaidiwa na watu kumlaza maiti. Hayo yalifanyika mara tatu. Imamu akawauliza jamaa zake iwapo yule maiti alikuwa mla riba na wakajibu ‘ndiyo’. Imamu akakataa kumsalia. Mwili wake ulipowekwa kaburini, ulizama. Watu walilifukia kaburi

na wakaondoka bila kutia fatiha. Tunajilinda kwa Allah عَزَّوَجَلَّ kutokana na ghadhabu yake.

Uovu wa riba

Ndugu waislamu! Matukio kama haya yanadhihirishwa ili watu wapate kuogopa matokeo mabaya ya kutenda dhambi na wafuate mienendo ya Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم.

Hata hivyo mbali na adhabu zinazodhihiri kwa watu, watenda dhambi wanaweza wakawa wanapewa adhabu kali zaidi. Katika kisa hicho maiti ameonyeshwa kuwa alikuwa ni mla riba. Bila shaka riba nayo inamaangamizi makubwa. Soma hadithi zifuatazo ili upate kuelewa:

1. Imetajwa katika *Ṣaḥīḥ Muslim*: Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amemlaani mwenye kupokea, mwenye kutoa, mwenye kushuhudia na mwenye kusajili mkataba wa riba na akasema: “Wote wako sawa.” *(Ṣaḥīḥ Muslim, uk. 862, hadithi 1598, Dār- Ibn-ul- Ḥazm, Beirut)*

2. Imetajwa katika *Sunan Ibn-e-Mājaĥ*: Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema: “Riba ina sehemu 73, sehemu ndogo kabisa ni ile ya mtu kuzini na mama yake.” *(Sunan Ibn-e-Mājaĥ, juz. 03, uk. 72, hadithi 2274-2275)*

3. Ikiwa mtu, kwa kujua, atapokea Dirham moja kwa njia ya riba, adhabu yake ni kali zaidi kuliko kuzini mara 36. *(Musnad Imām Aḥmad bin Ḥanbal, juz. 8, uk. 223, hadithi 22016, Dār-ul-Fikr, Beirut)*

4. Imetajwa katika *Sunan Ibn-e-Mājaĥ*: Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema: “Usiku wa Isra wal Miraj niliwaona watu ambao matumbo yao yalikuwa kama nyumba na ndani yake mlikuwa na nyoka walioonekana kwa nje. Nikamuuliza Jibril عَلَيْهِ السَّلَام “Hawa ni watu gani?” Akaniambia kuwa ni watu waliokuwa wakila riba.” *(Sunan Ibn-e-Mājaĥ, juz. 03, uk. 71-72, hadithi 2273, Dār-ul-Ma’rifaĥ, Beirut)*

Mfafanuzi maarufu wa Qur’an, Muftī Aḥmad Yār Khān Naeemī رَحْمَةُ اللهِ تَعَالٰى عَلَيْه alishereheshea hadithi hii: “Leo mnyoo mdogo akipatikana tumboni, anaathiri afya na hukosesha utulivu. Seuze yule ambaye tumbo lake limejaa nyoka na nge atasikia uchungu ulioje? Tunaomba stara ya Allah عَزَّوَجَلَّ. *(Mirāt-ul-Manājīĥ, juz. 4, uk. 259, machapisho ya Al-Qurān, Markaz-ul-Auliyā Lahore)*

5. Kaburi lilikuwa limejaa nge

Katika kijiji kimoja, kinyozi alikuwa katika sakaratul mauti. Watu walimwambia apige shahada[1] lakini hakupiga. Wakamwambia apige shahada tena lakini kwa sababu ya mateso ya mauti aliitukana shahada[2], muda mchache baadaye akafa. Alipokuwa ataka kuzikwa, kila mtu alipiga mayowe kwa sababu kaburi

[1] Njia sawa ni kuwa wale walioko karibu waiseme shahada kwa sauti kumkumbusha, wasimlazimishe.

[2] Imetajwa katika *Bahar-e-Shari’at* sehemu ya 4 uk 158 ikiwa mtu atatamka neno la kufuru wakati wa kutolewa roho hatahukumiwa kuwa kafiri kwa sababu inawezekana akawa ametamka hali ya kuwa amepoteza fahamu kwa uchungu wa umauti.

lake lilikuwa limejaa nge. Watu wakalifukia na wakachimba jingine lakini pia lilikuwa limejaa viumbe hao wakutisha. Hatimaye, walimzika hivyo hivyo. Tunajilinda kwa Allah عَزَّوَجَلَّ kutokana na ghadhabu yake.

Tumo kutokana na kunyoa ndevu ni haramu

Vinyozi watumao kwa kunyoa ndevu au kuzipunguza kinyume na sunna inafaa wapate funzo kutokana na kisa hicho. Ni haramu kuishi kwa kutegemea kazi kama hii. Inafaa waogope adhabu kali kutoka kwa Allah عَزَّوَجَلَّ wale wanaonyoa ndevu zao kinyume na sunna kwani kufanya hivyo ni haramu. Imetajwa katika *Waqār-ul-Fatāwā*, sehemu 1, uk 259: "Ni haramu kunyoa au kunyolewa ndevu, na mapato kutokana na kufanya hivyo ni haramu."

Hukumu ya uislamu kuhusu mali ya haramu

Kuna aina mbili ya mali ya haramu:

1. Mali ya haramu kutokana na wizi, hongo au njia nyingine yoyote ya haramu haiwezi kuwa yako. Hukumu ya sharia ni kuiregesha kwa mwenyewe. Iwapo amekufa, lazima wapewe warithi wake na ikiwa hawakupatikana basi itolewe kama sadaka bila ya nia ya kupata thawabu.

2. Mali inayopatikana kupitia ʻAqd-e-Fāsid (mapato kutokana na kazi ambazo haziruhusiwi; mfano riba, vinyozi wanaonyoa ndevu bila kuzingatia sunna nk.). Mali hii haiwezi kuwa

yako lakini si faradhi kuzirudisha kwa mwenyewe au warithi wake. Unaweza kuzitoa kama sadaka bila ya nia ya kupata thawabu lakini ni bora zaidi ukiregesha kwa mwenyewe au warithi wake. *(Fatāwā-e-Razawiyyaĥ, juz. 23, uk. 551-552)*

Baraka za Madanī kwa kujitolea kikweli kweli

Napenda kuwatolea kisa cha ajabu cha Madani kilichotokea kwa dada mmoja muislamu katika eneo la Mumbai, India. Baada ya kumalizika ijtimai ya kila wiki ya Dawat-e-Islami kwa kina dada iliyofanyika tarehe 22 Ṣafar-ul-Muẓaffar 1428 A.H (12 Machi 2007), dada mmoja mgeni katika uislamu alimwendea dada muislamu msimamizi na kumjulisha kuwa amepoteza viatu vyake. Dada msimamizi akavua viatu vyake na akataka kumpa. Dada mwengine, aliyekuwa ana karibu miezi saba tangu kujiunga na mazingira ya madani ya Dawat-e-Islami, aliposikia mazungumzo yao alisogea karibu na akasema, “Kwani siwezi kujitolea angaa kidogo kwa ajili ya Dawat-e-Islami?” Alivua viatu vyake na akamlazimisha dada mgeni avikubali na yeye akaenda nyumbani miguu chuma.

Alipokwenda kulala usiku alibahatika kumuota Mtume Kipenzi صَلَّى اللّٰهُ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم, uso wake ulikuwa unang’ara kama mwezi na katika miguu yake iliyobarikiwa amekaa Muballigh mzee wa Dawat-e-Islami akiwa amevaa kilemba cha kijani. Mtume Mtukufu صَلَّى اللّٰهُ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم akammiminia sifa nzuri kwa kusema, “Nimependezwa mno na maneno uliyoyasema wakati ulipojitolea

kutoa viatu vyako, yaani, “Kwani siwezi kujitolea angaa kidogo kwa Dawat-e-Islami?” (Mbali na hayo, Mtume Mtukufu صَلَّی اللّٰہ تَعَالٰی عَلَیْہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم alimmiminia mapenzi makubwa).

Ndugu waislamu! Je, unaweza kutambua baraka zinazotokana na kujitolea? Ubora wa kujitolea ni mkubwa mno na humkuza mtu katika daraja ambazo hawezi kudhania. Mtume Mtukufu صَلَّی اللّٰہ تَعَالٰی عَلَیْہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم amesema, “Mtu anayetoa akipendacho, atasamehewa na Allah عَزَّوَجَلَّ.” *(Ittaḥaf-us-Sādat-il-Muttaqīn, juz. 9, uk. 779, Dār-ul-Kutub-ul-‘Ilmiyyaĥ, Beirut)*

Ndugu waislamu! Je haiwezekani wewe kujitolea kusafiri na Madanī Qāfilaĥ kwa siku tatu tu kila mwezi ili ujitayarishie Ahera yako. Ina hitaji uzingativu mkubwa! “Hatuwezi kujitolea angaa kidogo kwa Dawat-e-Islami?”

Ewe Allah عَزَّوَجَلَّ! Tupe uwezo wa kujitolea kwa nia safi. Tujaalie mwisho mwema wakati wa mauti chini ya kuba lilobarikiwa katika mji mzuri wa Madīna-tul-Munawwaraĥ, tuzikwe katika Jannat-ul-Baqī na tuingizwe Peponi bila hesabu. Tujaalie kuwa majirani wa Kipenzi chako صَلَّی اللّٰہ تَعَالٰی عَلَیْہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم katika Jannat-ul-Firdaus.

اٰمِیْن بِجَاہِ النَّبِیِّ الْاَمِیْن صَلَّی اللّٰہُ تَعَالٰی عَلَیْہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم

صَلُّوْا عَلَی الْحَبِیْب صَلَّی اللّٰہُ تَعَالٰی عَلٰی مُحَمَّد

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ وَالصَّلٰوةُ وَالسَّلَامُ عَلٰى سَيِّدِ الْمُرْسَلِيْنَ اَمَّا بَعْدُ فَاَعُوْذُ بِاللّٰهِ مِنَ الشَّيْطٰنِ الرَّجِيْمِ بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

BLOSSOMING OF SUNNAH

By the grace of Allah عَزَّوَجَلَّ, Sunnahs are abundantly learnt and taught in the Madani environment of Dawat-e-Islami, a global and non-political movement for the preaching of Quran and Sunnah. It is a Madani request that you spend the whole night in the weekly Sunnah-Inspiring Ijtima', taking place after Salat-ul-Maghrib every Thursday in your city, for the pleasure of Allah عَزَّوَجَلَّ with good intentions. With the intention of gaining reward, make it a part of your routine to travel in Sunnah-Inspiring Madani Qafilahs with the devotees of Rasul, to fill out the Madani In'amat booklet every day practicing Fikr-e-Madinah and to submit it to the relevant responsible Islamic brother of your locality within the first ten days of every Islamic month. Through the blessings of this, you will develop a mindset and a yearning to adopt Sunnahs, to have hatred for sins and to protect your faith, بِجَاهِ النَّبِيِّ الْاَمِيْن عَزَّوَجَلَّ

Every Islamic brother should develop the Madani mindset that **'I must strive to reform myself and people of the entire world,** بِجَاهِ النَّبِيِّ الْاَمِيْن عَزَّوَجَلَّ"

In order to reform ourselves, we must act upon Madani In'amat and to strive to reform people of the entire world we must travel with Madani Qafilahs, بِجَاهِ النَّبِيِّ الْاَمِيْن عَزَّوَجَلَّ

MC 1288

Aalmi Madani Markaz, Faizan-e-Madinah, Mahallah Saudagaran
Purani Sabzi Mandi, Bab-ul-Madinah, Karachi, Pakistan.
UAN: +92 21 111 25 26 92 | Ext: 1262
Web: www.dawateislami.net | E-mail: translation@dawateislami.net